

## TANGAZO



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA  
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



Katibu Mtendaji, Baraza la Mitihani la Tanzania anapenda kuwajulisha watu wote wanaotarajia kufanya Mtihani wa **Kidato cha Sita (ACSEE)** mwezi **Mei 2024** kama Watahiniwa wa Kujitegemea kwamba;

1. Kipindi cha kawaida cha usajili wa Watahiniwa wa Kujitegemea kitakuwa kuanzia tarehe **01 Julai** hadi **30 Septemba, 2023** kwa ada ya Shilingi **50,000/=**. Aidha, watakaojisajili kwa **kuchelewa** yaani kuanzia tarehe **01 Oktoba** hadi **31 Oktoba, 2023** watalipa Shilingi **65,000/=** na hakutakuwa na usajili mwagine baada ya tarehe **31 Oktoba, 2023**.
2. Usajili utafanyika kwa njia ya mtandao (**online**). Aidha, kabla ya kujisajili, waombaji wanapaswa kwenda kwenye Vituo vya Mitihani kuchukua **Namba Rejea (Reference Number)** zinazotolewa bure na kufanya malipo ya ada kupitia Benki kwa kutumia 'Control Number'.
3. Ufafanuzi kuhusu utaratibu na hatua za kufuata katika kutengeneza '**Control Number**' na kujisajili, umetolewa katika tovuti ya Baraza la Mitihani la Tanzania: [www.necta.go.tz](http://www.necta.go.tz). Aidha, kwa watahiniwa ambao hawataweza kutumia mfumo huo wafike ofisi za Posta zilizo jirani nao.
4. Waombaji wote **wanasisitizwa** kuhakikisha wanajisajili mapema kwani mfumo wa usajili utafungwa baada ya kipindi cha usajili kukamilika.

Imetolewa na;

**KATIBU MTENDAJI**